Imetolewa: Jumanne 13 Oktoba 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MPANGO WA O.R. TAMBO KUHUSU VIGODA VYA UTAFITI AFRIKA: KUTANA NA TIMU INAYOLENGA KUFANYA MABADILIKO YA MAZINGIRA YA UTAFITI BARANI AFRIKA.

Pretoria Afrika ya Kusini: Mpango wa Vigoda vya Utafiti Afrika (Africa Research Chairs Initiative (ORTARChI), unayo furaha kukutaarifu kuwa imechagua taasisi kumi na watafiti wenyeviti ambao ni waanzilishi wa awamu ya kwanza ya programu hiyo. Mpango huu ulioanzishwa na Mfuko wa Utafiti wa Afrika ya Kusini (National Research Foundation - **NRF**) Idara ya Sayansi na Ubunifu (Department of Science and Innovation - **DSI**) kwa ushirikiano na Mfuko wa Oliver & Adelaide Tambo (OATF), Kituo cha Kimataifa cha Maendeleo ya Utafiti, Canada (Canada's International Development Research Centre - **IRDC**) na Mabaraza Saba ya Maendeleo ya Sayansi, yaliyoko kusini mwa jangwa la Sahara (seven councils of the Science Granting Councils Initiative in Sub-Saharan Africa - **SGCI**).

"Katika kipindi cha miaka 5 ijayo, Wenyeviti wa Vyuo Vikuu vya Umma kutoka mataifa saba ya Afrika (7) watafanya utafiti kwa kujenga uelewa mpana na kusaidia kukuza maendeleo ya ujuzi katika mada mbalimbali zikiwemo mada katika Hali ya hewa, Sekta ya Afya, Ujasiriamali na Ajira kwa Vijana. Kwa kupitia majumuisho ya dhana ya wenyeviti wa utafiti duniani, watafiti hawa katika madaraja ya kimataifa hawatazingatia tu mwingiliano wa timu mbalimbali pekee bali pia watawekeza nguvu zaidi katika kizazi kijacho cha utafiti," Alisema Dkt. Molapo Qhobela, Afisa Mtendaji Mkuu, NRF

ORTARChI hutoa ufadhili wa miaka mitano kwa takribani kiasi cha Dola za Kimarekani **milioni 15** kama ruzuku. Ruzuku hii hutolewa baada ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu na ukaguzi wa mchakato mzima kwa kuzingatia ubora wa taasisi na uwezo katika taaluma zilizoainishwa, kuongoza katika kufadhili tafiti zenye ubora na weledi. Wanufaika wengine ni pamoja mtafiti mmoja mmoja na watafiti wabobezi wanaofahamika katika ngazi ya kimataifa.

Aidha, pamoja na msaada wa ruzuku itakayotolewa kwa wanafunzi wa masomo ya uzamili na uzamivu (Postgraduate Students) na elimu baada ya udaktari (postdoctoral fellowship), fedha zitatolewa kupitia NRF na Mfuko wa Oliver & Adelaide Tambo (OATF) kwa wanafunzi wa kike hamsini na tano (55) wa Kiafrika wanaosomea shahada ya uzamivu chini ya usimamizi wa mpango huu. "Kupitia ushirikiano huu wa kimkakati wa Kimataifa na kikanda, Wenyeviti wa Vigoda watachangia maendeleo ya ushirikiano wa muda mrefu, kwa wanufaika wa pande zote katika bara la Afrika." Anaeleza Rais wa IDRC, Dkt. Jean Lebel.

MPANGO WENYEWE

Mpango huu umejengwa kutokana na kazi ya Oliver Tambo, Kiongozi Mashuhuri wa Afrika ya Kusini na Mwafrika nguli aliyebobea katika historia ya elimu ya sayansi, anayeamini mageuzi kupitia utoaji elimu, ushirikiano na mshikamano wa mataifa barani Afrika.

“Huu ni ukurasa mpya kwa mpango huu wa ORTAChi. Mpango huu kwa mara ya kwanza ulitangazwa mnamo mwaka 2017 katika maadhimisho ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa Kiongozi muhimu wa Afrika ya Kusini aliyepambania ukombozi wa Afrika. O.R Tambo ambaye aliongoza chama cha siasa cha Afrika kusini (African National Congress), wakati akiwa katika uhamisho nje ya nchi. O. R. Tambo hakuwa tu kiongozi wa kujitolea kwa Afrika, bali pia alikuwa ni mtetezi wa masuala ya sayansi na teknolojia” Anasema Zengeziwe Msimang, Ofisa Mtendaji Mkuu wa OATF.

Mpango huu wa ORTARChI ni fursa ya kukuza maadili ambayo yaliasisiwa na O.R. Tambo yanayozingatia Uadilifu, Ujasiri, Diplomasia na Unyenyekevu. O.R. Tambo pia anatambua jitihada za Afrika kama kitovu cha umahiri na kwamba Bara la Afrika litaendelea kuwa nyumba ya uvumbuzi na vipaji.

"Kujenga katika urithi huu wa O.R Tambo, ORTARChI itaongeza mfumo wa elimu ya juu, kukuza utafiti na maendeleo barani Afrika. Muhimu ni mchango wa Mpango huo katika kukuza ushirikiano wa kudumu katika nchi zilizo ndani na nje ya Afrika. Kwa pamoja, kigoda cha Utafiti pia kitaongeza ushirikiano na asasi za kiraia, sekta binafsi, na serikali, njia inayostahili kupongezwa kwa kutekeleza utafiti bora, "ameongeza Prof Vitória Langa de Jesus, Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Kitaifa wa Utafiti wa Msumbiji (FNI).

Ni heshima kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa viti viwili vya utafiti katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMAIST). Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Prof Gerald Misinzo na Prof. Hulda Swai kwa juhudi zao, ambazo zinachangia mabadiliko ya eneo la utafiti nchini Tanzania. Msaada wa kigoda cha Utafiti cha O.R. Tambo kimekuja wakati muafaka ambapo nchi imeingia kwenye uchumi wa kati. Msaada huo utashughulikia maswala muhimu katika jamii yetu kwa kuhakikisha usalama wa chakula, kupunguza ongezeko la vifo vinavyosababishwa na ugonjwa wa malaria, magonjwa ya wanyama na kujenga uhusiano mzuri kwa watafiti kwa kupitia hili inapongeza juhudi za Serikali za kujenga uchumi wa kitaifa na kujenga maisha bora na ustawi kwa watu wake 'Amosi Nungu - Mkurugenzi Mkuu Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH)

MUALIKO WA VYOMBO VYA HABARI

Washiriki kutoka Vyombo vya Habari na umma kwa ujumla mnakaribishwa katika ufunguzi rasmi wa Kigoda cha utafiti mnamo tarehe 27 Oktoba, 2020 kama sehemu ya Sherehe za Kumbukizi ya kuzaliwa kwa O.R. Tambo. Tukio litafanyika kwa njia ya Mtandao ambapo kutakuwa na meza ya mazungumzo ikiendeshwa na Waziri wa Sayansi na Ubunifu wa Afrika ya Kusini, Dkt. Blade Nzimande ikiambatana na kumbukumbu ya miaka 103 ya kuzaliwa kwa O.R Tambo.

Kwa Taarifa zaidi kuhusu programu ya Kigoda cha Utafiti Afrika cha O.R Tambo.
Tarehe: 27 Oktoba 2020
Siku: Jumanne,
Muda: Kuanzia Saa 8:30 mchana Mpaka saa 10:30 jioni
Jisajili sasa uweze kushiriki, Bofya kihunzi kifuatacho
http://nrf.ac.za/or_tambo_africa_research_chairs_initiative_launch

WENYEVITI WETU

Ifuatayo ni orodha kamili ya wenyeviti 10 wa utafiti na taasisi waandaaji waliochaguliwa na ORTARChI

M/KITI WA UTAFITI	**TAASISI NA NCHI**	**ENEO LA MADA**	**MTAZAMO WA M/KITI WA UTAFITI**
Prof. Gizaw Mengistu Tsidu	Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Sayansi na Teknolojia Botswana *(Botswana International University of Science & Technology, Botswana)*	Mabadiliko ya Tabia Nchi. (*Climate change)*	Mabadiliko ya hali ya hewa na mapokeo katika rasilimali za maji, mimea na mifugo. (*Climate change and adaptation in water, vegetation and livestock resources)*
Prof. Almeida Sitoe	Chuo Kikuu cha Eduardo Mondlane Msumbiji. (*Eduardo Mondlane University, Mozambique)*	Mabadiliko ya Tabia Nchi (*Climate change)*	Mifumo ya ikolojia kwa maeneo ya nusu ukame na ukame (Ecosystems for arid and semi-arid zones)
Prof. Samiratou Ouedraogo and Prof Olga Lompo	Chuo Kikuu cha Ouaga Ipr Joseph KiZerbo, Burkina Faso *(University Ouaga I-Pr Joseph KiZerbo, Burkina Faso)*	Sayansi ya Afya (*Health Sciences)*	Saratani na Afya kwa Umma (*Cancer and public health)*
Prof. Kwesi Saalia	Chuo Kikuu Cha Ghana *(University of Ghana)*	Usalama wa Chakula *(Food Security)*	Udhibiti Ubora na Usalama wa chakula *(Food safety and quality)*
Prof. Nathaniel Boso	Kwame Nkrumah Chuo Kikuu cha Sayansi na	Uchumi na Biashara	Ujasiriamali na Ajira kwa Vijana

M/KITI WA UTAFITI	TAASISI NA NCHI	ENEO LA MADA	MTAZAMO WA M/KITI WA UTAFITI
	Teknolojia (*Kwame Nkrumah University of Science and Technology, Ghana)*	*(Business and economics)*	(*Entrepreneurship and youth employment)*
Prof. Gerald Misinzo	Chuo Kikuu Cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro Tanzania (*Sokoine University of Agriculture, Tanzania)*	Usalama wa Chakula. *(Food Security)*	Afya ya Mifugo (*Livestock health)*
Prof. Noble Banadda	Chuo Kikuu cha Makerere Uganda (*Makerere University, Uganda)*	Usalama wa Chakula. *(Food Security)*	Kilimo endelevu *(Sustainable agriculture)*
Prof. Stephen Syampungani	Chuo Kikuu cha Copperbelt, Zambia (*Copperbelt University, Zambia)*	Nishati *(Energy)*	Nishati Asilia na mimea (*Bioenergy and biofuels)*
Prof. Imasiku Nyambe	Chuo Kikuu cha Zambia (*University of Zambia)*	Utafiti wa Maji (*Water Research)*	Udhibiti wa Ubora na Vyanzo vya Maji (*Water quality and catchment protection)*
Prof. Hulda Swai	Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, Arusha Tanzania *(African Institution of Science and Technology, Tanzania)*	Teknolojia ya Nanotechnology	Utoaji wa dawa Kuzuia Malaria (*Anti-malarial drug delivery)*

WENYEVITI WA VIGODA VYA UTAFITI NI AKINA NANI?

Hawa ni wenyeviti wataalamu ambao huteuliwa kwa kutambua mchango binafsi, kujitolea na vipaji vyao katika vyuo vikuu ili kusaidia katika tafiti zenye ubora wa hali ya juu. Sifa kuu ya wenyeviti huongeza hamasa kwa watu binafsi katika kuchochea utaalamu kwenye eneo mtambuka na kufundisha kwa vizazi vijavyo vya wasomi, sambamba na kuvutia uhifadhi wa vipaji bora vya utafiti katika taasisi fulani.

Wenyeviti hutarajia kufikia malengo yaliyowekwa kwa maendeleo ya wafanyakazi, lakini pia fedha za ziada hutolewa kwa wanafunzi mara baada ya masomo ya udaktari na uzamivu chini ya usimamizi wa wenyeviti husika. Vituo hivi vya utafiti vinaathiri maendeleo ya ukuzaji wa miundombinu ya utafiti katika nchi wenyeji, kwa kutoa mchango wa uzalishaji elimu (Maarifa na Ujuzi) wa hali ya juu kwa kuoanisha na Ajenda ya Umoja wa Afrika (Africa Union) ya mwaka 2063 na Mkakati wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Afrika (STISA 2024).

Waanzilishi wa Kigoda cha programu ya Utafiti ya Canada (Canada's pioneering Canada Research Chairs programme) ilianzishwa mnamo mwaka 1997 na imeshafadhili Vigoda vya Utafiti visivyopungua 2,000 kupitia utaratibu huo mpaka sasa. Mpango wa Mafanikio ya Kigoda cha Utafiti cha Afrika ya Kusini (The Successful South African chairs initiative – SARChi) ulianzishwa mnamo mwaka 2006, kama mkakati wa kuwakutanisha Serikali ya Afrika ya Kusini kwa kuwavutia na kuendelea kusimamia ubora katika Tafiti na ubunifu kwa vyuo vikuu vya umma vya Afrika ya Kusini, Mabaraza ya Utafiti na vituo vya kitaifa vya utafiti. Vievile, SARChi kupitia uwezeshaji wake umelenga kuongeza uwezo wa kitafiti kwa kuendeleza ukuaji wa uwezo binafsi na kutoa hamasa kwa ukuzaji wa maarifa kwa kizazi kipya. SARChi pia inajikita kusaidia na kukuza mageuzi ya jamii ya watu wa Afrika ya Kusini kidemografia na maarifa ya kiuchumi, ili kujenga usawa na ushiriki wa Pamoja katika ukuzaji wa maarifa na hatimae yaweze kutafasiriwa kwa kuonesha faida za uchumi wa kijamii. Utekelezaji wa programu ya ORTARChi umeunganishwa na SARChi ili kutoa nafasi ya kubadilishana uzoefu na ushirikiano endelevu miongoni mwa watafiti bora barani Afrika.

MWISHO

Maswali kwa Vyombo vya Habari yawasilishwe kwa:

Candice Molefe
Meneja: Mawasiliano na Vyombo vya Habari
Tume ya Utafiti Afrika ya Kusini (NRF)
Simu: +27(0) 12 481 4054 / +27 72 485 0725
Barua pepe: candice.molefe@nrf.ac.za

Natasha Allie
Meneja mawasiliano na Mradi
Taasisi ya Oliver & Adelaide Tambo
Simu. +27(0) 11880 2680/+27 82 4226547
Barua pepe: natasha@tambofoundation.org.za

KUHUSU NRF:

Mfuko wa Utafiti ya Afrika ya kusini (National Research Foundation) ni taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa Utafiti. Ina jukumu la kusaidia na kuendeleza tafiti kupitia ufadhili, ukuzaji wa rasilimali watu na utoaji wa vifaa vya ulazima katika ufanyaji tafiti ili kuzalisha maarifa, ubunifu na kukuza kada ya sayansi na teknolojia, ikiwemo maarifa ya wazawa, kusaidia na kukuza uelewa kwa jamii na ushiriki katika sayansi, na kuendeleza na kuimarisha mfumo wa kitaifa wa Sayansi pamoja na kusaidia vipaumbele vya Serikali na hatimaye kuwezesha usawa wa maisha kwa watu wa Afrika ya Kusini.
Tovuti: www.nrf.ac.za | Twitter: @NRF_News | Facebook: @NRFSouthAfrica.

KUHUSU OATF:

Mwaka 2020 ni mwaka wa mafanikio kwa Taasisi ya Oliver & Adelaide. Kumbukizi ya miaka 60 tangu familia ya Tambo kuishi nje ya nchi, miaka 30 ya kurudi Afrika ya Kusini, na miaka 10 tangu kuanzishwa kwa Taasisi ya Tambo. Taasisi Oliver na Adelaide Tambo ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kusimamia, kulinda na kuhifadhi heshima ya wapigania uhuru na demokrasia, Oliver na Adelaide Tambo. Taasisi imekuwa ikisimamia kumbukizi ya Tambo kwa kuwezesha eneo la elimu, kuinua jamii kupitia mpango wa kuwainua wanawake na kuwezesha vijana kufahamu thamani ya Tambo. Tunaamini kuwa thamani ya Tambo katika uadilifu, uwajibikaji, nidhamu, uafrika, na ujumuishi wa maadili ya viongozi ni muhimu katika kuzingatia demokrasia na kuwapatia vijana uongozi na silaha ya kusisitiza ilitunikiwa na Tambo kuilinda Afrika ya Kusini na Afrika kwa kizazi kijacho.
Tovuti: www.tambofoundation.org.za| Twitter / Facebook / Instagram: @TamboFoundation

KUHUSU IDRC

Kituo cha Kitaifa cha Utafiti cha Maendeleo Canada IDRC hufadhili tafiti katika nchi zinazoendelea ili kukuza maendeleo, kupunguza umaskini, na kufanya mabadiliko kwa kiwango kikubwa. Tunaunga mkono juhudi za wataalam ambao wanaoongoza kuendeleza maarifa na kutatua changamoto za maendeleo kwa vitendo. Tunawawezesha rasilimali, ushauri, na mafunzo wanayohitaji katika kutekeleza na kushiriki kwenye matokeo yao ya suluhisho za changamoto zao. Kwa kifupi, IDRC imeongeza fursa - na kufanya mabadiliko yenye utofauti katika jamii.
Tovuti: https://www.idrc.ca/en | Twitter: @IDRC_CRDI | Facebook: @IDRC.CRDI

KUHUSU SGCI

Mpango wa Mabaraza ya Sayansi katika Jumuiya ya Kusini mwa Jangwa la Sahara (SGCI) ni mpango wa wafadhili wengi ambao unakusudia kuimarisha uwezo wa mabaraza 15 yanayotoa sayansi huko Kusini mwa Jangwa la Sahara ili kusaidia sera za utafiti na msingi wa ushahidi ambao utachangia uchumi na maendeleo ya kijamii.
Tovuti: https://sgciafrica.org/en-za/home | Twitter: @SGCIAfrica